

Ni kwa namna gani, upendo husitiri wingi wa dhambi? (1Petro 4:8).

Tusome,

1 Petro 4:8 “Zaidi ya yote iweni na juhudini nyingi katika kupendana; kwa sababu upendano husitiri wingi wa dhambi”.

Awali ya yote ni muhimu kufahamu maana ya neno “kusitiri” na vile vile ni muhimu kufahamu ni nani ambaye anayesitiriwa dhambi zake, je! ni yule anayependa au anayependwa?

Neno “**kusitiri**” maana yake “**kufunika au kuficha**”..mtu aliyevaa nguo za kuufunika mwili wake wote, maana yake “kavaa nguo za kujisitiri mwili wake, ili asibakie kuwa tupu”. (Kauficha mwili wake).

Sasa tukirudi kwenye huo mstari wa kwenye **1Petro 4:8**, maandiko yanasema upendano husitiri wingi wa dhambi.

Sasa dhambi *zinazositiriwa/kufichwa* si za yule anayependa bali yule anayependwa.

Sasa zinasitiriwa kwa namna gani?

Ni kwa namna gani, upendo husitiri wingi wa dhambi? (1Petro 4:8).

Neno la Mungu linasema katika kile kitabu cha *1Wakorintho 13:4-5*.

1 Wakorintho 13:4 “Upendo huvumilia, hufadhili; upendo hauhusudu; upendo hautakabari; haujivuni;

5 haukosi kuwa na adabu; hautafuti mambo yake; hauoni uchungu; hauhesabu mabaya; Mwisho kabisa anasema “UPENDO HAUHESABU MABAYA”.

Kutokuhesabu mabaya ndio **“Kusitiri dhambi”**.

Maana yake ni kwamba mtu mwenye upendo, maisha yake yote ni ya kusamehe tu na kutoweka kumbukumbu ya mambo mabaya anayofanyiwa.

Mathayo 18:21 “Kisha Petro akamwenda akamwambia, Bwana, ndugu yangu anikose mara ngapi nami nimsamehe? Hata mara saba?

Ni kwa namna gani, upendo husitiri wingi wa dhambi? (1Petro 4:8).

22 Yesu akamwambia, Sikuambii hata mara saba, bali hata saba mara sabini”.

Mfano mzuri wa Mmoja aliyeweza kusitiri wingi wa dhambi nyingi, ni Bwana wetu Yesu Kristo mwenyewe.

Kwa Upendo wake mwingi alijitoa nafsi yake sadaka ili sisi tupate kusitiriwa dhambi zetu. Kwake yeye tumepata ondoleo la dhambi. Tukiwa dhani yake hatuhukumiwi.

Mtume Paulo anazidi kuliweka wazi hilo katika kitabu cha Warumi.

Warumi 4:7 “Heri waliosamehewa makosa yao, Na waliositiriwa dhambi zao.

8 Heri mtu yule ambaye Bwana hamhesabii dhambi”.

Je na wewe leo dhambi zako zimesitiriwa na kuondolewa kabisa??

Ni kwa namna gani, upendo husitiri wingi wa dhambi? (1Petro 4:8).

Kumbuka dhambi zako haziwezi kuondolewa kama haupo ndani ya pendo la Kristo, kwasababu ni upendo tu ndio unaositiri wingi wa dhambi, maana yake kama haupo ndani upendo wa Kristo, basi hauna msamaha wa dhambi.

Sasa utauliza, unaingiaje katika pendo hilo na kupata msamaha?.

Unaingia katika pendo hilo kwa kutubu dhambi zako zote kwa kumaanisha kuziacha, na kubatizwa katika ubatizo sahihi wa jina la Yesu Kristo na kumpokea Roho Mtakatifu.

Baada ya hapo dhambi zako zote zitaondolewa na kuwa mrithi wa ahadi za Mungu.

Na vile vile unapowahubiria wengine habari za Pendo la Kristo, na hata wao wakaingia katika pendo hilo, (kwa kutubu na kuacha dhambi)basi utakuwa umewasaidia dhambi zao kufunikwa na pia kuwaokoka na adhabu ya ziwa la moto, sawasawa na maandiko yafuatayo.

Yakobo 5:19 “Ndugu zangu, ikiwa mtu wa kwenu amepotelea mbali na kweli, na mtu mwingine akamrejeza;

Ni kwa namna gani, upendo husitiri wingi wa dhambi? (1Petro 4:8).

20 jueni ya kuwa yeye amrejezaye mwenye dhambi hata atoke katika njia ya upotevu, ataokoa roho na mauti, na kufunika wingi wa dhambi.

Bwana atubariki sote.

Maran atha!

Tafadhali washirikishe na wengine habari hizi njema,

Kwa maombezi/Ratiba za ibada/ Ushauri/ Maswali.

Piga namba hizi: +255693036618 au +255789001312

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge na channel yetu kwa kubofya link hii

>> <https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10>

Mada Nyinginezo:

Ni kwa namna gani, upendo husitiri wingi wa dhambi? (1Petro 4:8).

UPENDO NI NINI NA JE! KUNA AINA NGAPI ZA UPENDO?

JE UPENDO WAKO UMEPOA?

UPENDO WA MUNGU.

UPENDO WA KRISTO WATUBIDISHA;

JE UPENDO WAKO UMEPOA?

Rudi nyumbani

Share on:

WhatsApp